Q1

OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI ZANZIBAR

MAKAO MAKUU YA POLISI ZANZIBAR

# TOLEO LA ROBO MWAKA LA TAKWIMU ZA AJALI NA MAKOSA YA BARABARANI ZANZIBAR

## JANUARI – MACHI 2026

OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI ZANZIBAR

## Utangulizi

Ripori hili hutolewa kila baada ya robo mwaka na hukusanya takwimu za toleo la kila mwezi za ajali na makosa ya barabarani. Ripoti hii ni muhtasari wa takwimu za maeneo mawili ya uhalifu ambazo ni ajali na makosa ya barabarani. Takwimu hizi zinatolewa kwa kutofautiana kwa kijiografia, kimakundi na kijinsia.

Takwimu za ajali barabarani hutoa taarifa za idadi ya ajali zilizotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ajali. Takwimu za makosa ya barabarani hutoa taarifa kuhusu makosa ya barabarani ambayo yameainishwa katika makundi makuu kumi na moja (11).

## Lengo

Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ajali na makosa ya barabarani za ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu na hutumiwa na wapangaji, watunga sera, nawatoa maamuzi.

## Ajali za Barabarani


Jumla ya ajali 100 zimeripotiwa kwa mwezi Januari - Machi mwaka 2026. Wilaya ya Kati imeripotiwa kuwa na ajali nyingi (ajali 19) sawa na asilimia 19.0 ikilinganishwa na wilaya nyengine.

**Kielelezo 1.1: Idadi ya Ajali za Barabarani Kwa Wilaya; Januari - Machi, 2026**





Jumla ya waathirika 134 wameripotiwa kwa mwezi wa Januari - Machi 2026, ambapo waathirika 120 ni wanaume na waathirika 14 ni wanawake. Wilaya ya Kaskazini 'B' imeripotiwa kuwa na waathirika wengi (waathirika 27) sawa na asilimia 20.1 ikilinganishwa na wilaya nyengine.

**Kielelezo 1.2: Idadi ya Waathirika wa Ajali za Barabarani, Januari - Machi 2026**





Jumla ya waathirika 65 wameripotiwa kufariki kwa ajali za barabarani mwezi Januari - Machi 2026, ambapo waathirika 61 walikuwa wanaume na waathirika wanne (4) wanawake. Wilaya ya Magharibi 'B' imeripotiwa kuwa na waathirika wengi waliofariki (waathirika 13) sawa na asilimia 20.0 ikilinganishwa na wilaya nyengine.

**Kielelezo 1.3: Idadi ya Waathirika Waliofariki kwa Ajali za Barabarani, Januari - Machi 2026**





Jumla ya waathirika 69 wameripotiwa kujeruhiwa kwa ajali za barabarani mwezi Januari - Machi 2026, ambapo waathirika 59 walikuwa wanaume na waathirika 10 wanawake. Wilaya ya Kaskazini "B" imeripotiwa kuwa na waathirika wengi waliojeruhiwa (waathirika 20) sawa na asilimia 29.0 ikilinganishwa na wilaya nyengine.

**Kielelezo 1.4: Idadi ya Waathirika Waliojeruhiwa wa Ajali za Barabarani, Januari - Machi 2026**





Miongoni mwa waathirika wa ajali za barabarani (waliojeruhiwa na waliofariki) kwa mwezi wa Januari - Machi 2026 , waathirika wengi wameonekana walikuwa wapanda baiskeli na pikipiki 64, wakifuatiwa na abiria 42, waenda kwa miguu waathirika 19 na madereva walikuwa waathirika 9.

**Kielelezo 1.5: Idadi ya Waathirika wa Ajali za Barabarani, Januari - Machi 2026**





Ajali nyingi zilizoripotiwa kwa mwezi wa Januari - Machi 2026 zilitokea muda wa saa 12:01 jioni hadi saa 03:00 usiku ambapo zimeripotiwa ajali 28

**Kielelezo 1.6: Idadi ya Ajali za Barabarani na Muda Uliotokea, Januari - Machi 2026**




Jumla ya ajali za barabarani 65 kati ya ajali 100 zilizoripotiwa kwa mwezi wa Januari - Machi 2026, zimesababishwa na kuendesha gari kwa mwendo kasi na ajali 35 zimesababishwa na uzembe wa dereva. Mkoa wa Mjini Magharibi umeripotiwa kuwa na ajali nyingi zilizosababishwa na kuendesha gari kwa mwendo kasi (ajali 22) na Uzembe wa madereva (ajali 14).

**Kielelezo 1.7: Chanzo cha Ajali za Barabarani kwa Mkoa, Januari - Machi 2026**




## Makosa ya Barabarani

Jumla ya makosa 25,809 ya barabarani yameripotiwa kwa mwezi wa Januari - Machi 2026, ambapo makosa 25,796 yameripotiwa kwa wanaume na makosa 13 yameripotiwa kwa wanawake.

Wilaya ya Magharibi 'A' imeripotiwa kuwa na idadi kubwa ya makosa ya barabarani (makosa 5,013) sawa na asilimia 19.4 kati ya makosa yote yaliyoripotiwa. Wilaya ya Micheweni ina idadi ndogo ya makosa ya barabarani yaliyoripotiwa ambayo ni makosa 180 (asilimia 0.7) kati ya makosa yote yaliyoripotiwa.


**Kielelezo 2.0: Idadi ya Makosa ya Barabarani Kwa Wilaya, Januari - Machi 2026**




Kosa kuu lililoripotiwa mwezi Januari - Machi 2026 lilikuwa Kutokufuata miongozo na kanuni za usalama barabarani (makosa 8,264) yakifuatia Kuzidisha idadi ya abiria na mizigo (makosa 6,502) na Kuendesha chombo cha moto (gari/vespa/pikipiki/fifti) bila ya leseni, bima na leseni ya njia (makosa 3,944).

Orodha ya makosa haya matatu (3) ya barabarani kati ya yote kumi (10) yaliyoripotiwa mwezi Januari - Machi 2026 yamechangia asilimia 72.5.

**Kielelezo 2.1: Idadi ya Makosa ya Barabarani, Januari - Machi 2026**



## HITIMISHO

Takwimu za ajali barabarani hutoa taarifa za idadi ya ajali zilizotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ajali. Takwimu za makosa ya barabarani hutoa taarifa kuhusu makosa ya barabarani ambayo yameainishwa katika makundi makuu kumi na moja (11). Lengo la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ajali na makosa ya barabarani za ndani ya Zanzibar.

Jumla ya ajali 100 zimeripotiwa kwa mwezi Januari - Machi mwaka 2026. Wilaya ya Kati imeripotiwa kuwa na ajali nyingi (ajali 19) sawa na asilimia 19.0 ikilinganishwa na wilaya nyengine

Jumla ya waathirika 134 wameripotiwa kwa mwezi Januari - Machi 2026, ambapo waathirika 120 ni wanaume na waathirika 14 ni wanawake.

Jumla ya makosa 25,809 yameripotiwa Januari - Machi 2026, ambapo makosa 25,796 yameripotiwa kwa wanaume na makosa 13 yameripotiwa kwa wanawake.

Kosa kuu lililoripotiwa kwa Januari - Machi 2026 ni Kutokufuata miongozo na kanuni za usalama barabarani (makosa 8,264) sawa na asilimia 32.0 ya makosa yote yaliyoripotiwa Januari - Machi 2026.

## KIAMBATANISHO:

**Jadweli 1: Idadi na Asilimia ya Waathirika Walioripotiwa kwa Ajali za Barabarani kwa Wilaya na Jinsi; Januari - Machi 2026**

| Wilaya | Idadi ya Ajali | | Waliokufa | | | | Waliojeruhiwa | | | | Jumla | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Nambari | Asilimia | Wanaume | Wanawake | Jumla | Asilimia | Wanaume | Wanawake | Jumla | Asilimia | Wanaume | Wanawake | Jumla | Asilimia |
| Kaskazini 'A' | 9 | 9.0 | 7 | 0 | 7 | 10.8 | 5 | 0 | 5 | 7.2 | 12 | 0 | 12 | 9.0 |
| Kaskazini 'B' | 12 | 12.0 | 7 | 0 | 7 | 10.8 | 13 | 7 | 20 | 29.0 | 20 | 7 | 27 | 20.1 |
| Kati | 19 | 19.0 | 9 | 0 | 9 | 13.8 | 12 | 2 | 14 | 20.3 | 21 | 2 | 23 | 17.2 |
| Kusini | 6 | 6.0 | 5 | 0 | 5 | 7.7 | 1 | 0 | 1 | 1.4 | 6 | 0 | 6 | 4.5 |
| Mjini | 8 | 8.0 | 3 | 1 | 4 | 6.2 | 7 | 0 | 7 | 10.1 | 10 | 1 | 11 | 8.2 |
| Magharibi 'A' | 13 | 13.0 | 8 | 0 | 8 | 12.3 | 6 | 1 | 7 | 10.1 | 14 | 1 | 15 | 11.2 |
| Magharibi 'B' | 15 | 15.0 | 11 | 2 | 13 | 20.0 | 2 | 0 | 2 | 2.9 | 13 | 2 | 15 | 11.2 |
| Wete | 5 | 5.0 | 4 | 0 | 4 | 6.2 | 2 | 0 | 2 | 2.9 | 6 | 0 | 6 | 4.5 |
| Micheweni | 4 | 4.0 | 1 | 0 | 1 | 1.5 | 4 | 0 | 4 | 5.8 | 5 | 0 | 5 | 3.7 |
| Chake chake | 4 | 4.0 | 2 | 1 | 3 | 4.6 | 4 | 0 | 6 | 8.7 | 6 | 1 | 7 | 5.2 |
| Mkoani | 5 | 5.0 | 4 | 0 | 4 | 6.2 | 3 | 0 | 0 | 0.0 | 7 | 0 | 7 | 5.2 |
| **Zanzibar** | **100** | **100** | **61** | **4** | **65** | **100** | **59** | **10** | **69** | **100** | **120** | **14** | **134** | **100** |

**Jadweli 2: Idadi ya Waathirika Walioripotiwa kwa Ajali za Barabarani kwa Wilaya na Jinsi; Januari - Machi 2026**

| Wilaya | Idadi ya Ajali | Dereva | | | | | | Abiria | | | | | | Wapanda Baskeli na Pikipiki | | | | | | Waendao kwa Miguu | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Waliokufa | | | Waliojeruhiwa | | | Waliokufa | | | Waliojeruhiwa | | | Waliokufa | | | Waliojeruhiwa | | | Waliokufa | | | Waliojeruhiwa | | |
| | | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T | M | F | T |
| Kaskazini 'A' | 9 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 4 | 0 | 4 | 4 | 0 | 4 | 1 | 0 | 1 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 12 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 | 7 | 5 | 12 | 3 | 0 | 3 | 5 | 2 | 7 | 2 | 0 | 2 | 1 | 0 | 1 |
| Kati | 19 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 7 | 2 | 9 | 7 | 0 | 7 | 2 | 0 | 2 | 2 | 0 | 2 | 1 | 0 | 1 |
| Kusini | 6 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 | 0 | 5 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 8 | 2 | 0 | 2 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 1 | 3 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 3 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 13 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 3 | 0 | 3 | 2 | 0 | 2 | 3 | 0 | 3 | 5 | 0 | 5 | 0 | 1 | 1 |
| Magharibi 'B' | 15 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 | 4 | 0 | 0 | 0 | 6 | 1 | 7 | 2 | 0 | 2 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Wete | 5 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 4 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 3 | 0 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chake chake | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 | 4 | 0 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 5 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 2 | 0 | 2 | 2 | 0 | 2 | 1 | 0 | 1 |
| **Zanzibar** | **100** | **5** | **0** | **5** | **4** | **0** | **4** | **10** | **1** | **11** | **24** | **7** | **31** | **33** | **1** | **34** | **28** | **2** | **30** | **13** | **2** | **15** | **3** | **1** | **4** |

**Jadweli 3: Makosa ya Barabarani Yaliyoripotiwa Kwa Wilaya na Jinsi, Januari - Machi 2026**

| Wilaya | Watumiaji wa Ulevi/Vidonge | | | Uendeshaji Hatari | | | Ubovu wa Vipando | | | Kuendesha chombo cha moto bila ya kuvaa helmenti (vespa/pikipiki/fifti) | | | Kuendesha chombo cha moto (gari/vespa/pikipiki/fifti) bila yaleseni, bima na leseni ya njia | | | Kuzidisha idadi ya abiria na mizigo | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 19 | 0 | 19 | 10 | 0 | 10 | 0 | 0 | 0 | 245 | 0 | 245 | 1,001 | 0 | 1,001 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 3 | 10 | 0 | 10 | 159 | 0 | 159 | 1,269 | 0 | 1,269 |
| Kati | 0 | 0 | 0 | 275 | 0 | 275 | 117 | 0 | 117 | 113 | 0 | 113 | 315 | 0 | 315 | 332 | 0 | 332 |
| Kusini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 45 | 0 | 45 | 84 | 0 | 84 | 427 | 0 | 427 | 665 | 0 | 665 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 63 | 0 | 63 | 1,305 | 0 | 1,305 | 430 | 0 | 430 | 772 | 0 | 772 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 30 | 0 | 30 | 755 | 0 | 755 | 1,170 | 0 | 1,170 | 1,426 | 0 | 1,426 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 38 | 0 | 38 | 683 | 0 | 683 | 856 | 0 | 856 | 712 | 0 | 712 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 24 | 0 | 24 | 84 | 0 | 84 | 31 | 0 | 31 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 43 | 0 | 43 | 75 | 0 | 75 | 49 | 0 | 49 |
| Chake chake | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 184 | 7 | 191 | 75 | 0 | 75 | 79 | 0 | 79 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 86 | 6 | 92 | 108 | 0 | 108 | 166 | 0 | 166 |
| **Zanzibar** | **0** | **0** | **0** | **299** | **0** | **299** | **306** | **0** | **306** | **3,287** | **13** | **3,300** | **3,944** | **0** | **3,944** | **6,502** | **0** | **6,502** |

Inaendelea… Jadweli 3: Makosa ya Barabarani Yaliyoripotiwa kwa Wilaya na Jinsi, Januari - Machi 2026

| Wilaya | Kushindwa kuandika anuani yammiliki wa gari | | | Kughushi nyaraka za serikalikwa gari za abiria | | | Kushindwa kuvaa sare na beji kwa utingo na dereva kwa gariza abiria | | | Kutofuata miongozo na kanuniza usalama barabarani | | | Kupakia Mtu zaidi ya Wawilikwenye Chombo za Maringi Mawili | | | Jumla | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 129 | 0 | 129 | 1,701 | 0 | 1,701 | 16 | 0 | 16 | 3,121 | 0 | 3,121 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 289 | 0 | 289 | 2,404 | 0 | 2,404 | 8 | 0 | 8 | 4,142 | 0 | 4,142 |
| Kati | 210 | 0 | 210 | 195 | 0 | 195 | 309 | 0 | 309 | 165 | 0 | 165 | 182 | 0 | 182 | 2,213 | 0 | 2,213 |
| Kusini | 20 | 0 | 20 | 0 | 0 | 0 | 390 | 0 | 390 | 10 | 0 | 10 | 2 | 0 | 2 | 1,643 | 0 | 1,643 |
| Mjini | 433 | 0 | 433 | 0 | 0 | 0 | 244 | 0 | 244 | 1,347 | 0 | 1,347 | 0 | 0 | 0 | 4,594 | 0 | 4,594 |
| Magharibi 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 130 | 0 | 130 | 1,502 | 0 | 1,502 | 0 | 0 | 0 | 5,013 | 0 | 5,013 |
| Magharibi 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 228 | 0 | 228 | 893 | 0 | 893 | 0 | 0 | 0 | 3,410 | 0 | 3,410 |
| Wete | 12 | 0 | 12 | 0 | 0 | 0 | 109 | 0 | 109 | 103 | 0 | 103 | 0 | 0 | 0 | 365 | 0 | 365 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 7 | 0 | 7 | 6 | 0 | 6 | 0 | 0 | 0 | 180 | 0 | 180 |
| Chake chake | 13 | 0 | 13 | 10 | 0 | 10 | 104 | 0 | 104 | 64 | 0 | 64 | 40 | 0 | 40 | 571 | 7 | 578 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 114 | 0 | 114 | 69 | 0 | 69 | 0 | 0 | 0 | 544 | 6 | 550 |
| **Zanzibar** | **688** | **0** | **688** | **205** | **0** | **205** | **2,053** | **0** | **2,053** | **8,264** | **0** | **8,264** | **248** | **0** | **248** | **25,796** | **13** | **25,809** |

**Jadweli 3.7 Tozo zilizolipwa Mahakamani Kwa Wilaya na Idadi ya kesi, Januari - Machi 2026**

| Wilaya | Idadi ya kesi | Tozo(Shilingi) |
|---|---|---|
| Kaskazini 'A' | 2,189 | 60,438,900 |
| Kaskazini 'B' | 3,170 | 82,591,500 |
| Kati | 1,958 | 62,779,500 |
| Kusini | 1,193 | 42,734,350 |
| Mjini | 3,203 | 98,541,590 |
| Magharibi 'A' | 3,901 | 111,349,800 |
| Magharibi 'B' | 2,527 | 85,333,860 |
| Wete | 292 | 7,504,400 |
| Micheweni | 192 | 3,785,000 |
| Chake chake | 641 | 12,355,600 |
| Mkoani | 484 | 8,665,500 |
| Zanzibar | 19,750 | 576,080,000 |

## Zingatia Maelezo

Ajali za barabarani ni ajali yeyote iliotokea barabarani inayohusisha angalau chombo kimoja (chenye maringi mawili, matatu au manne). Kutokana na Sheria ya Adhabu nambari.6/2004 kuondoa Amri ya Adhabu, sura ya 13 ya sheria ya Zanzibar (Penal Act no. 6/2004 Act to repeal the Penal Decree, chapter 13 of the law of Zanzibar)

Kifo imefafanua iwapo kama watu wamepata ajali na kufa papo hapo au ndani ya mwaka mmoja na siku moja (366) baada ya ajali.

Watu waliojeruhiwa na waathirika kwa ajali waliopatwa na mshtuko wanaohitaji matibabu ya Hospitali au bila hospitali.

Njia kimsingi ina maana ya usafiri. Hio humpa binadamu kufikia maeneo tofauti. Watu wengi hutumia njia tofauti za usafiri. Baadhi yao hutumia gari, baiskeli na kwa miguu.

Kosa ni uhalifu ambao huvunja sheria fulani na kuwepo adhabu maalum. Ajali za barabarani husababishwa na makosa mbalimbali ya binadamu. Makosa mengi ambayo yanaonekana kuwa ni madogo lakini athari yake inakuwa kubwa. Matokeo yake watu hupata ulemavu au kufa.

**KWA UFAFANUZI ZAIDI TAFADHALI WASILIANA NA:**

**OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI**
Sanduku la Barua, 2321,
Simu: +255242231869,
Barua pepe: zanstat@ocgs.go.tz
Website: http://www.ocgs.go.tz

**MAKAO MAKUU YA POLISI ZANZIBAR**
Sanduku la Barua, 237,
Barua pepe:cidphqznz@gmail.com,
Nukushi: 024223136,
MMP, Zanzibar